**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**
DAR ES SALAAM
Namba ya Simu:0738166703
Fax: 255 - 022 – 246011
*e-mail*: secretary@psc.go.tz
***Website: www.psc.go.tz***

TUME YA UTUMISHI WA UMMA,
6 MTAA WA LUTHULI,
KITALU NA. 10,
S.L.P. 9143,
**DAR ES SALAAM.**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.

### RUFAA 107 NA MALALAMIKO 08 YA WATUMISHI WA UMMA YAMETOLEWA UAMUZI NA TUME

Tume ya Utumishi wa Umma leo tarehe 02 Julai 2021 imehitimisha Mkutano wa Nne wa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika Mkutano huu Tume ilipokea na kutolea uamuzi rufaa **107** na malalamiko **08** yaliyowasilishwa na Watumishi wa umma ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka zao za Ajira na Mamlaka za Nidhamu. Tume pia imejadili taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Robo ya 3 ya mwaka wa fedha 2020/2021. Mkutano huu wa Tume, umefanyika kwa muda wa wiki mbili na uliongozwa na Mwenyekiti wa Tume, Mheshimiwa Jaji (Mstaafu) Dkt. Steven James Bwana.

Katika mkutano huu wa Nne kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Tume imeshughulikia masuala yafuatayo:-

**Kupokea na kutoa uamuzi wa Rufaa 107**. Tume ilijadili na kutoa uamuzi wa rufaa 107, ambapo rufaa **76** zilikataliwa, rufaa **09** zilikubaliwa bila masharti na rufaa **12** zilikubaliwa kwa masharti kuwa mashauri hayo yaanzishwe upya kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo. Rufaa **10** zilikatwa nje ya muda, hivyo zilitupiliwa mbali na Tume.

**Kupokea na kutoa uamuzi wa malalamiko 08**. Tume ilipokea na kutolea uamuzi malalamiko 08 kati ya hayo malalamiko **03** yalikataliwa. Malalamiko **05** yalikubaliwa bila masharti.

*Makosa waliyotuhumiwa kutenda na yaliyosababisha baadhi ya watumishi wa umma kuchukuliwa hatua za nidhamu ni*;

i. Utoro kazini kwa zaidi ya siku 5 bila ruhusa ya Mwajiri;
ii. Watumishi kwenda masomoni bila ruhusa ya Mwajiri;
iii. Kutoa taarifa za uongo kwa Mwajiri;
iv. Kuajiriwa katika Utumishi wa Umma bila kuwa na sifa;
v. Kughushi cheti cha uhitimu wa Elimu ya Kidato cha Nne, Kushindwa kuwasilisha cheti cha Kidato cha 4.
vi. Kukosa uaminifu,
vii. Ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha ya umma.
viii. Uzembe uliokithiri na kushindwa kutekeleza majukumu.

Aidha, katika kipindi cha miaka miwili (2) 2019/2020 na 2020/2021, Tume imeshughulikia na kutolea jumla ya **rufaa 626** kati ya hizo **rufaa 219** zilikubaliwa, **rufaa 227** zilikataliwa na **rufaa 180** zilikatwa nje ya muda. Katika kipindi hicho Warufani **153** walipinga uamuzi wa Tume kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matokeo ya rufaa hizo yanaonesha kuwa hadi sasa jumla ya **rufaa 59** zimetolewa uamuzi na kati ya hizo **rufaa 52** amekubaliana na uamuzi wa Tume na **rufaa 7** amekataa kwa kutengua uamuzi wa Tume. Aidha, **rufaa 94** bado hazijatolewa uamuzi.

Katika Mkutano huu, Tume ilipokea na kuijadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari – Machi, 2021) ya mwaka 2020/2021. Miongoni mwa majukumu yaliyotekelezwa katika kipindi hiki ni kupokea na kushughulikia Rufaa **99** na Malalamiko **06;** Ukaguzi wa uzingatiaji wa masuala ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa umma ulifanyika na kutoa elimu kwa umma.

Kupitia taarifa hii Tume ilibaini masuala yafuatayo:-

i. Ucheleweshaji wa vielelezo vya rufaa na malalamiko;

ii. Kuchelewesha au kutowasilishwa kwa taarifa ya hali ya Utumishi wa umma.

***Masuala yaliyobainika;*** Tume katika kushughulikia na kutoa uamuzi wa rufaa na malalamiko yaliyowasilishwa mbele yake, ilibaini kuwepo kwa ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo miongoni mwa Watumishi wa Umma, na baadhi ya Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu. Baadhi ya masuala yaliyobainika ni:-

a) Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu kushindwa kuwachukulia hatua kwa wakati na kwa mujibu wa Sheria watumishi walio chini yao wenye utendaji usioridhisha.
b) Upungufu katika uandaaji wa mashtaka na uendeshaji wa mchakato mzima wa mashauri ya nidhamu.
c) Baadhi ya Mamlaka za Nidhamu kutokuunda Kamati za Uchunguzi au kutotumia Taarifa za uchunguzi wa awali kama zilivyowasilishwa kwao.
d) Kufungua mashauri ya nidhamu na kukaa nayo muda mrefu bila kuyahitimisha.
e) Baadhi ya Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma, warufani na waleta malalamiko kutoambatisha vielelezo.
f) Baadhi ya Waajiri kutokuzingatia maelezo ya Serikali katika kushughulikia masuala ya watumishi wao, hususan waliohusika katika zoezi la uhakiki wa vyeti.
g) Baadhi ya Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu bado zinachelewesha kuwasilisha na zingine haziwasilishi taarifa za masuala ya Rasilimali Watu kwa kila robo (miezi 3) ya mwaka wa fedha husika na kuikosesha Serikali uwezo wa kujitathmini jinsi ya uendeshaji wa masuala ya kiutumishi.

***Masuala yanayosisitizwa na Tume:***

Tume ya Utumishi wa Umma, leo inahitimisha Mkutano wa Nne kwa mwaka 2020/2021 kwa kusisitiza mambo yafuatayo:-

a) Watumishi wa Umma, Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu wanapaswa wakati wote kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayotolewa na Serikali.

b) Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu wanatakiwa kutekeleza maagizo ya Tume na ikiwa ni pamoja na kuwasilisha vielelezo vinavyohusiana na rufaa na malalamiko kwa wakati pale wanapotakiwa kufanya hivyo na Tume.

c) Kamati za Uchunguzi zinazoundwa na Mamlaka za Nidhamu kuchunguza tuhuma wanazokabiliwa nazo watumishi wa umma zinatakiwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kamati hizi zinatakiwa kufanya kazi yake kwa weledi mkubwa ili kuthibitisha au kutothibitisha tuhuma zinazowakabili watuhumiwa.

d) Mamlaka za Nidhamu zinapaswa kuwa makini katika uandishi wa Hati ya mashtaka, kurejea vipengele sahihi kuhusu tuhuma zinazowakabili watumishi wanaotuhumiwa kutenda makosa.

e) Waajiri wanatakiwa kushughulikia masuala ya kinidhamu ya watumishi wanaotuhumiwa kufanya makosa kwa wakati ili hatua stahiki zichukuliwe na ikithibitika kuwa hawana makosa wastaafu kwa heshima.

f) Watumishi wa umma wanapaswa kuzingatia utoaji wa taarifa sahihi wakati wa kujaza fomu za taarifa zao binafsi na Fomu za mfumo wa wazi wa Mapitio na Tathmini ya utendaji Kazi (OPRAS), wakidanganya au wakitoa taarifa zisizo sahihi watachukuliwa hatua.

g) Watumishi wote wa Umma wanapaswa kuzingatia Kanuni za Maadili katika utumishi wao na kutoa huduma bora kwa wananchi.

**Imetolewa na:-**

Richard M. Cheyo
MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
TUME YA UTUMISHI WA UMMA
DAR ES SALAAM
02 Julai, 2021